## KUHUSU MWANDISHI



Johanitha Jeremiah Ernest ni mwalimu wa vijana mwandishi, na mwalimu wa Neno la Mungu katika maeneo ya kusudi, maono, na kusikia sauti ya Mungu. Johanitha ni mwanzilishi wa taasisi ya vijana inayoitwa Visionary youth organization, pia ni mwanzilishi wa Jsmart digiTech.

## KUHUSU KITABU “URITHI WA MWANAUME IMARA"

**URITHI WA MWANAUME MWENYE NGUVU**
**Mafunzo 17 ya Maisha kwa Ajili ya Kijana wa Kiume**

Kuna nguvu kubwa inayotegemewa kutoka kwa mwanamume, lakini pia kuna vita kubwa inayomwandama. Dunia ya sasa inapita katika mabadiliko yanayomfanya kijana wa kiume kupoteza mwelekeo wa nafasi yake ya asili kama kiongozi, mlinzi, na nguzo. Ukweli ni kwamba, shetani ana vita ya makusudi na uzao wa kiume; anajua mwanamume akidhoofika, msingi wa familia na jamii unaporomoka.

Katika kitabu hiki, Johanitha Jeremiah Ernest anashirikisha hekima alizozipata kupitia maisha ya shujaa wake baba yake, Engineer Jeremiah Ernest. Kwa miaka saba sasa tangu baba yake alipokumbwa na changamoto ya afya iliyomfanya ashindwe kuendelea na kazi, Johanitha amekuwa akijifunza kwa kusikia sauti yake ya hekima, kutazama, na kupata uzoefu wa maisha kutoka kwa jamii iliyomzunguka.
Mwandishi anatamani sauti hii ya baba isinyamae, bali iendelee kupaza ndani ya mioyo ya vijana ili kutengeneza kizazi imara kitakachosimama dhidi ya kila hila na kurejesha utawala wa mwanamume.

**Ndani ya kurasa hizi, utajifunza mengi ikiwamo:**

- Kushinda Vita ya Hatima: Jinsi ya kuilinda nafasi yako kama kuhani na kiongozi kupitia misingi ya kiroho.
- Utawala wa Kiuchumi: Siri za umiliki wa rasilimali na uwekezaji wa ardhi kama silaha ya ukombozi.
- Misingi ya Chuma: Kujenga utu na nidhamu itakayokulinda hata wakati wa dhoruba za maisha.
- Urithi wa Milele: Jinsi ya kuacha alama inayozungumza kwa vizazi vijavyo kupitia maadili na bidii.

Kijana, simama kwenye nafasi yako. Huu ni urithi wako; upokee, uishi, na uukabidhi kwa kizazi kijacho.

ISBN 978-9912-42-322-0
9 789912 423220



Johanitha Jeremiah
+255 746 003 974
johanithajeremiah@gmail.com